

HALMASHAURI YA WILAYA YA RUFUJI.

MKOA WA PWANI:  
SIMU 023 2010304  
Fax 023 2010317  
Email: [dedrufiji@gmail.com](mailto:dedrufiji@gmail.com)



S. L.P 28,  
UTETE/RUFUJI.

*Unapojibu tafadhali taja:  
(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W))*

18/09/2017.

**TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA UDEREVA KATIKA KITUO CHA  
AFYA NYAMINYWILI.**

Mkurugenzi Mtendaji (W) anawatangazia wananchi wote wa Wilaya ya Rufiji wenye sifa kuomba nafasi tajwa hapo juu kwa ajili ya kuendesha gari la wagonjwa.

**Masharti ya kibali cha ajira.**

- i. Wenye sifa tu ndio waombe nafasi hiyo.
- ii. Ajira hii itakuwa ya mkataba wa mwaka mmoja mmoja.
- iii. Mshahara utaanzia **ngazi ya TGOS A**, kima cha kuanzia ni sh. 328,000/ kwa mwezi.

**Sifa za Mwombaji:**

- i. Awe na elimu ya kidato cha IV na kuendelea.
- ii. Awe na leseni ya udereva **class D**
- iii. Awe amepata mafunzo ya udereva kutoka katika chuo kinachotambulika na Serikali
- iv. Awe na umri usiozidi miaka 45.

**Kazi za kufanya (Majukumu).**

- i. Kusafirisha wagonjwa waliopewa rufaa kutoka kituo cha afya Nyaminywili hadi hospitali ya Wilaya au sehemu nyingine.
- ii. Kuhakikisha gari na vyombo vyake vipo katika hali nzuri wakati wote, na kufanya uchunguzi wa gari kabla na baada ya safari ili kugundua ubovu unaohitaji matengenezo.
- iii. Kufanya matengenezo madogo madogo katika gari.
- iv. Kutunza na kuandika daftari la safari (log book) kwa safari zote.

Maombi yote yatumwe kwa anwani ifuatayo:  
Mkurugenzi Mtendaji (W)  
S. L. P 28  
**UTETE/ RUFJI.**

Mwisho wa kupokea maombi ni siku kumi na nne (14) tangu tarehe ya tangazo hili.



Eng. Frobert Andrea.  
Kny. Mkurugenzi Mtendaji (W)  
**RUFJI.**

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA RUFJI**